

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA

Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji

SMU. +255 (028) 2220 287,

Faksi: 0282221839

E-mail: ded@bukobadc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja :

Kumb.KGR/ BDC/T.1/1/156

S.L.P. 491

BUKOBA

9.08.2021



TANGAZO LA ZABUNI YA KUKODISHA MAGARI - TOYOTA LAND CRUISER HARDTOP NA HIACE

Halmashauri ya Wilaya Bukoba inakaribisha maombi ya zabuni kutoka kwa mtu binafsi au kikundi chochote mwenye/chenye gari/magari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP AU HIACE**. Kwa ajili ya kufanya kazi maalum kuanzia tarehe 07/9/2020 hadi tarehe 09/9/2020.

Masharti kwa mwombaji:-

1. Gari liwe na cheti cha ukaguzi kutoka kwa Mamlaka husika.
2. Mwombaji aambatanishe namba ya utambulisho ya Mlipakodi wa Serikali (TIN namba).
3. Mwombaji aambatanishe nakala ya kadi ya gari husika.
4. Malipo yatafanyika kuitia akaunti ya mwombaji
5. Gari linatakiwa kuwa na BIMA ya gari iliyo hai.
6. Gari linatakiwa liwe na sanduku la vifaa (toolbox).
7. Gari linatakiwa liwe na kizimia moto ambacho hakijaisha muda wake wa matumizi (fire extinguisher).
8. Gari linatakiwa liwe na magurudumu yaliyo katika hali nzuri na uwepo wa gurudumu la akiba (Spare tyre).

9. Gari linatakiwa liwe na viakisi mwanga viwili (Reflectors).
10. Mwombaji aandike namba ya simu katika barua ya maombi kwa ajili ya mawasiliano.
11. Mwombaji atakayekidhi vigezo na kuchaguliwa atajaza mkataba na Halmashauri wa kufanya kazi hii kwa siku tatu na gari litapangiwa kufanya kazi hiyo katika eneo lolote katika Halmashauri ya Wilaya.
12. Waombaji wote watataarifiwa juu ya matokeo ya maombi hayo kwa barua

Maombi yatumwe kwa **Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya, S.L.P 491, Bukoba.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 17/08/2021 saa 9.30 Alasiri.

morega
MOREGA S. MONGATE
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA**
*: MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P 491
BUKOBA*